BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 09 Juni, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

239. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na katazo la kuegesha vyombo vya moto baina ya njia ya *round about* ya Michenzani hadi Mlandege. Kadhia hiyo imesababisha wakaazi, wafanyabiashara na wateja kukosa maeneo ya kutosha ya kuegesha vyombo vyao pamoja na kutembea masafa marefu kuegesha vyombo hivyo.

(a) Je, Serikali imewapangia maeneo gani rafiki mbadala ya kuegesha vyombo hivyo kwa wakaazi, wafanyabiashara na wateja wa maeneo hayo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kutafuta na kujenga *parking* za kudumu kwa ajili ya wakaazi, wafanyabiashara na wateja wa maeneo hayo.

**<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>**

75. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wananchi wa Magomeni wanaishukuru na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa ujenzi wa miradi ya BIG Z katika jimbo hilo hasa barabara za ndani. Hata hivyo, miradi hii imekuja na changamoto kubwa za Wasimamizi wa Miradi (Consultants) wanaosimamia miradi hiyo kurundika vifusi katika majumba ya watu, kutokamilisha uzibaji wa mitaro, kuchelewa kuwalipa fidia wananchi waliopata matatizo ya nyumba na mengineyo.

(a) Je, Serikali inazielewa vipi changamoto hizo wanazopitia wananchi wa Magomeni.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi hao.

350. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipago:

Chanzo kikuu cha fedha cha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ni michango kutoka kws wanachama wake ambao ni wafanyakazi wote walioajiriwa katika sekta rasmi waliopo Zanzibar, na fedha hizo tumeshuhudia zinawekezwa katika miradi mbalimbali.

(a) Je, kwa sasa ZSSF ina jumla ya wanachama wangapi, na wanakusanya jumla ya mapato ya kiasi gani kwa mlinganisho wa mwezi na mwaka.

(b) Wanachama wachangiaji wanafaidika vipi na uwekezaji huu unaofanywa na ZSSF kupitia fedha za wanachama wake.

**<u>Wizara ya Kazi na Uwekezaji:</u>**

148. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Je, Wizara ina mfumo gani wa kufuatilia na kuhakikisha wawekezaji wanatekeleza wajibu wao kwa jamii, ikiwemo kulipa kodi stahiki na kulinda mazingira.

521. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la

Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Katika kuhakikisha Serikali inatekeleza miradi yake kama ilivyopangwa kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money), uwazi na kuepusha utekelezaji usioridhisha ili kulinda fedha za umma ni muhimu sana;

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha miradi ya ubia baina ya sekta za umma na binafsi inatekelezwa ipasavyo.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

347. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa skuli nyingi za binafsi za msingi na maandalizi ni skuli zilizo katika nyumba za watu binafsi, ambazo zinafahamika kama skuli nyumba na tayari Serikali imepiga marufuku skuli za aina hizo.

(a) Je, Serikali imefanya tathmini ipi ya kujua ni skuli ngapi ambazo zitafungiwa kwa kuwa ni skuli zenye muelekeo wa skuli nyumba.

(b) Je, ni idadi ya wanafunzi wangapi wanaotoka katika skuli hizo.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

317. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Ucheleweshaji wa upimaji na usajili wa ardhi umechangia kuongezeka kwa migogoro isiyo ya lazima na kupunguza uhakika wa umiliki wa ardhi kwa wananchi.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuharakisha zoezi la upimaji wa ardhi pamoja na utoaji wa hatimiliki kwa wananchi ili kuongeza uhakika wa umiliki wa ardhi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha mifumo ya usajili na utambuzi wa ardhi kwa kutumia teknolojia za kisasa.

531. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Mipango Miji inazingatia ongezeko la watu katika kisiwa cha Unguja na Pemba.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

278. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifungo:

Imebainika kwamba mbinu zinazotumika kulinda Maliasili za Misitu yetu ni za kizamani sana, jambo linalowapa wakati mgumu watumishi wa Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, hasa ikizingatiwa kuwa hawana silaha wala mafunzo, kwani Idara nzima kuna mtu mmoja tu aliyewahi kupatiwa mafunzo hayo.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha mfumo wa ulinzi unaboreshwa ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo watumishi hao, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi pasipo na usumbufu wowote.

525. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa wakulima wetu tumewahamasisha na wamehamasika katika kilimo cha mboga mboga kama vile Tungule, bado tunaendelea kushuhudia wakati wa mavuno, Tungule zinakuwa nyingi sana, hali inayopelekea kushuka kwa bei.

Je, Serikali imejipangaje kuzuia kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

214. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la ujenzi na uanzishaji wa vituo vya mafuta (Petrol Stations) maarufu kama sheli, karibu sana na nyumba za makaazi ya wananchi, jambo ambalo ni hatari inapotokezea ajali za moto katika vituo hivyo.

Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na suala hilo.

523 MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembe Samaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa Zanzibar inategemea umeme kutoka Tanzania Bara;

Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mrefu wa kujitegemea katika

uzalishaji wa nishati ya umeme.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

132. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Naipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa pencheni jamii kwa wazee waliofikia miaka 70.

(a) Je, ni wazee na familia ngapi za Watu Wenye Ulemavu zimeingizwa katika programu hiyo hadi sasa.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha wazee na familia za Watu Wenye Ulemavu hawa wanaoishi katika mazingira magumu.

(c) Je, Watu Wenye Ulemavu Mkubwa na Watu Wenye Ulemavu wa Akili wanazingatiwa vipi katika programu hiyo.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

74. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nane imewekeza sana kwenye ujenzi wa viwanja vya kisasa ambavyo ni moja ya kichocheo muhimu cha vijana kushiriki michezo.

Je, Serikali ipo tayari kiasi gani kurudisha hadhi na hamasa ya ligi hizo za vijana kwa kutumia viwanja hivyo vyenye hadhi, ili kutanua wigo wa michezo na kuchochea fursa za ajira kwa kuunga mkono lengo la Serikali la ajira 300,000

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

53. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa ipo miradi ya ujenzi wa barabara za ndani zinazoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

(a) Je, Serikali inatambua vipi athari kubwa za uharibifu wa miundombinu ya mifumo ya maji, umeme na makaazi ya watu kutokana na ujenzi wa barabara zinazoendelea kujengwa.

(b) Je, ni upi wajibu wa mkandarasi pindi anapoharibu miundombinu hiyo na kusitisha huduma muhimu kwa wananchi.

220. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Pamoja na ukweli wa gari za Serikali kukusudiwa kutumiwa kwa matumizi tu ya shughuli za Serikali na katika wakati maalum, baadhi ya magari hayo hutumiwa hata usiku wa manane na kinyume na taratibu za shughuli za Serikali.

(a) Ni upi muda wa kuanza kutumiwa na kulazwa kwa magari ya Serikali.

(b) Je, Serikali imetoa muongozo wowote wa gari zake kulazwa nje ya maeneo ya Ofisi za Serikali.

(c) Serikali imefanya tathmini gani na kugundua kutumiwa kwa baadhi ya magari yake kinyume na matumizi yanayotakiwa.

<u>**Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda:**</u>

522. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Duniani kote Zanzibar inajuulikana kuwa ni kisiwa cha karafuu, kwa maana ya wingi wa uzalishaji wake, uzuri na zenye ubora wa hali ya juu. Hata hivyo, tafiti zinaonesha kuwa uzalishaji wa karafuu katika visiwa vya Unguja na Pemba umepungua.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuongeza uzalishaji wa karafuu katika kisiwa cha Unguja na Pemba.

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuweka mazingira mazuri, ili kuhakikisha karafuu zetu tunazitumia wenyewe katika shughuli mbalimbali za utekelezaji wa bidhaa badala ya kuzisafirisha kama 'Raw Materials'.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**

402. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Tehknolojia ya Habari na Ubunifu:

Tokea mkonga wa mawasiliano utandikwe katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar, ni muda mrefu sasa umepita huduma ya mawasiliano ya mtandao huo hayajaleta faida iliyotarajiwa hapa nchini. Huduma za mtandao wa "internet" inayotolewa kupitia mkonga inapatikana katika baadhi ya maeneo ya mjini na mengine haijafika kabisa.

(a) Kwa nini huduma ya mtandao kupitia mkonga wa mawasiliano ina suasua hapa Zanzibar hata kwa maeneo ya Mjini.

(b) Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha kuwa huduma ya mawasiliano ya mkonga inafika kila kona ya visiwa vya Zanzibar.

(c) Je, Serikali kwa kushirikiana na TTCL itafanya vipi kuhakikisha Jiji lote la Zanzibar linakuwa na huduma ya "*internet*" kupitia mkonga, sambamba na huduma hiyo kufikishwa maeneo mengine visiwani.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

224. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Wizara ilipanga kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Mahamamu Kijichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni pamoja na kuimarisha Mradi wa Eneo la Kihistoria Maruhubi Unguja.

Je, kuna sababu gani zilizopelekea maeneo hayo kutotekelezwa.

346. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hifadhi ya maeneo ya Jozani ni miongoni mwa maeneo muhimu ya kivutio cha utalii hapa Zanzibar. Sehemu ya eneo hilo inamilikiwa na wananchi mbalimbali ambao hulitumia kwa kufanya shughuli zao za kilimo kwa mujibu wa masharti na miongozo ya hifadhi.

Je, wananchi hao wanafaidika vipi na maeneo yao kuwa sehemu ya

kivutio cha utalii.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

502. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Vikundi vya ushirika ni chombo muhimu katika kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umaskini. Hata hivyo, bado kuna haja ya kuimarisha usajili, uendeshaji na uendelevu wa vikundi hivyo, ili viweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa wananchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha na kuongeza usajili wa vikundi vya ushirika kiteknolojia katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuvijengea uwezo vikundi hivyo, ili viweze kujiendesha kwa tija na misingi ya kibiashara.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

328 MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Pamoja na juhudi za Serikali za kuwawezesha wananchi wanaojishughulisha na shughuli za uchumi wa buluu kuwapatia mitaji, bado wananchi hawa wanakabiliwa na changamoto zinazopunguza uendelevu na tija ya shughuli hizo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za kitaalamu na ufuatiliaji endelevu ili kuhakikisha wananchi hao wanapata tija inayotarajiwa.

**Wizara ya Afya:**

285. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamekuwa tatizo sugu kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Wataalamu wa Afya kufika mijini na vijijini kutoa elimu ya afya, ili wananchi waweze kutambua

mapema dalili za awali za magonjwa hayo na kuwahi kupata uchunguzi na matibabu.

506. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kupunguza vifo vya watoto ni miongoni mwa viashiria muhimu vya ubora wa huduma za afya na ustawi wa jamii.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kupunguza vifo vya watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano Zanzibar.

(b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kuimarisha huduma za kinga, lishe na matibabu kwa watoto katika vituo vya afya na hospitali.

(c) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kufuatilia maeneo yenye viwango vya juu vya vifo vya watoto, ili kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

389. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kuna walimu wanaoendelea kujiendeleza kielimu hadi kufikia Shahada ya Uzamili (Master) na Shahada ya Uzamivu (PhD), isipokuwa kwamba, marekebisho ya mishahara yao bado haipo wazi.

(a) Je, sera ya Serikali inasema vipi kuhusu marekebisho ya mishahara kwa walimu wanaomaliza masomo yao katika Shahada hizo na huku wakiwa bado wapo kazini.

(b) Je, kuna usahihi upi kwa walimu waliyomaliza Shahada ya Uzamili kuongezewa kiasi kidogo (mfano Tsh. 50,000) bila ya kuzingatia hadhi ya elimu hiyo.

Zanzibar,
09 Juni, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR